

TANZANIA

HESAWA

THE CHATO CONVENTION
ON
SCHOOL HEALTH AND SANITATION
(17TH - 28TH MAY 1992)

PROCEEDINGS AND RECOMENDATIONS



LIBRARY
INTERNATIONAL REFERENCE CENTRE
FOR COMMUNITY WATER SUPPLY AND
SANITATION SERVICES

Compiled by: **M.M. Kishumba**
A. Lukwatage (Mrs)
S. M. Kunaga

Facilitated by: **Dr. E. S. Mwasha**
AMREF Health Advisor for HESAWA

TABLE OF CONTENTS

	PAGE
1. INTRODUCTION.....	1
Workshop objectives.....	1
Participants' expectations....	1
2. TIME SCHEDULE AND MAIN SUBJECTS OF THE WORKSHOP.....	3
3. LIST OF PARTICIPANTS.....	5
4. GENERAL OBSERVATIONS.....	6
5. CHAPTER ONE: Recommendations on the VHWS and Revolving Fund study done by the Health Advisor	7
6. CHAPTER TWO: Recommendations on the School Health and Sanitation Package compiled by the Health Advisor	14
7. CHAPTER THREE: Recommendations on SIDA's Guidelines on Environmental Hygiene	16
8. CHAPTER FOUR: Recommendations regarding latrines and the Revolving Fund	21
9. CHAPTER FIVE: Miscellaneous Issues -	
i) Sustainability of Sanitation activities after HESAWA has phased-out	23
ii) COBASHECA Club	24
iii) Strengthening the role of TBAs	25
iv) Follow up seminars at Regional level	25

LIBRARY, INTERNATIONAL REFERENCE
CENTRE FOR COMMUNITY WATER SUPPLY
AND SANITATION (IWC)
P.O. Box 95193, 2509 AD The Hague
Tel. (070) 814911 ext. 141/142

ISBN 13062

LO: 203.2 92HF

APPENDICES

- Appendix 1 Short notes on LePSA method
- Appendix 2 School Health Clubs
- Appendix 3(a) Introductory remarks on the school health
and sanitation package
- Appendix 3(b) Facilitators' notes for the school health
education programme
- Appendix 4 Evaluation of the workshop by participants
- Appendix 5 Concluding remarks by the Health Advisor

WARSHA YA WALIMU WA WALIMU WA WAV (MIKOA NA WILAYA)
KANDA YA ZIWA - CHATO

INTRODUCTION

Warsha ya RTOTs na DTOTs kutoka mikoa mitatu ya Mwanza, Mara na Kagera hufanyika mara moja kila mwaka kujadili mafanikio , matatizo na kulinganisha utekelezaji wa mradi wa WAV na Usafi wa Mazingira katika mpango wa HESAWA.

Warsha ya Chato iliyofanyika kuanzia tarehe 17 Mei 1992 hadi 30 Mei 1992 ilijumuisha RTOTs wote na DTOTs wawili toka kila wilaya yenye mradi ambapo DTOTs 15 kati yao waluinda kikundi kimoja na waliobaki waliunda kikundi kingine.

Kikundi cha DTOTs 15 kilifanya kazi ya mafunzo kwa vitendo na kingine kiliendelea na warsha ya kawaida ya kila mwaka.

Kikundi kilichoendelea na warsha ya kawaida kilianza kazi yake kwa kuweka uongozi wa warsha chini ya Mwenyekiti Nd. F. B. Kalimanzira RHO Mara. Ratiba pia ilipangwa na washiriki wote wa warsha.

Madhumuni ya warsha:

Madhumuni ya warsha yalikuwa haya yafuatayo:

- a) Kujadili matokeo ya utafiti juu ya utendaji kazi wa WAV pamoja na usafi wa mazingira uliofanyika April 92, kujadili matatizo na kutafuta ufumbuzi wake.
- b) Kujadili jinsi ya kutekeleza mpango wa Elimu ya Afya mashuleni kama chanzo cha kuelimisha wananchi.
- c) Kujadili mfumo wa upimaji maji, utumiaji wa madawa katika maji (disinfection) pamoja na utoaji taarifa juu ya shughuli hizo.
- d) Kujifunza na kujenga aina mbalimbali za vyoo ikiwa ni pamoja na choo aina ya Bwina.

Madhumuni hayo yaliyoana sawa na matarajio ya wanawarsha ambayo yalikuwa kama ifuatavyo.

- a) Kupata taarifa za mafanikio kutoka mikoa yote mitatu ya mradi wa HESAWA.
- b) Kusahihisha fikra potovu za watu kuhusu vyoo katika mwadi wa HESAWA

- c) Kupata matatizo yanayokwamisha utekelezaji wa sera ya usafi wa mazingira na ufumbuzi wake.
- d) Kujadili hatua za kusimamia na kufanikisha shughuli za usafi wa mazingira katika mradi.
- e) Kuona na kujifunza ujenzi wa vyoo aina ya Bwina
- f) Fikra, mila na desturi zinazokwamisha utekelezaji wa usafi wa mazingira na hasa katika ujenzi wa vyoo.
- g) Kuona sababu zinazokwamisha mfuko wa mzunguko (revolving fund).
- h) Kujua aina ya vyoo vinavyohitajika katika mradi wa HESAWA.
- i) Kujua shughuli za usafi wa mazingira zitaendaje baada ya HESAWA kujiondoa - phasing-out.
- j) Kujua matatizo yanayowakabili WAV na kutafuta ufumbuzi wake.
- k) Kujadili matatizo juu ya upimaji maji.
- l) Kutafuta mbinu mbalimbali za kukabiliana na tatizo la vifo vya akina mama na watoto.
- m) Kutafuta mbinu za kuharakisha ongezeko la WAV ili kufikia lengo la Taifa.
- n) Kujua jinsi ya kuratibu shughuli za HESAWA pamoja na wahisani wengine.

SHUGHULI ZA KILA SIKU

TAREHE	SHUGHULI
17/5/92	<ol style="list-style-type: none"> 1. Utangulizi, kujitambulisha, kujiandikisha 2. Mipango ya utawala katika semina (climate setting)
18/5/92	<ol style="list-style-type: none"> 1. Madhumuni ya semina 2. Matarajio ya wanasemina 3. Majadiliani kwa vikundi juu ya Usafi wa Mazingira kwa kuzingatia kabrasha la Dr. E. S. Mwasha juu ya "Study on Revolving Fund and VHWS Performance Report".
19/5/92	<ol style="list-style-type: none"> 1. Majadiliano ya vikundi yaliendelea.
20/5/92	Kikao cha pamoja (Plenary session)
20/5/92	<ol style="list-style-type: none"> 1. Kusoma matokeo ya majadiliano ya vikundi 2. Kujadili matokeo ya majadiliano kwa vikundi 3. Uchambuzi wa mwisho juu ya matokeo ya majadiliano (angalia sura ya kwanza)
21/5/92	<p>Kikao cha pamoja (plenary session)</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Utangulizi juu ya School Health Package 2. Utumiaji wa LEPSA ana PBL tunaposhirikisha jamii katika kutatua matatizo yao 3. Mjadala juu ya School Health Package 4. Majadiliano katika vikundi juu ya SHP ili kuangalia utekelezaji wake katika mradi wa HESAWA (angalia sura ya pili)
22/5/92	<ol style="list-style-type: none"> 1. Kusoma matokeo ya mjadala juu ya School Health Package 2. Uchambuzi wa mwisho juu ya School Health Package (angalia sura ya pili) 3. Mazoezi juu ya kutumia LEPSA wakati wa kufundisha watu wazima.
25/5/92	<ol style="list-style-type: none"> 1. Majadiliano juu ya kabrasha la "SIDA Guidelines on Environmental Sanitation" (angalia sura ya tatu).

- 26/5/92
1. Mjadala juu ya takwimu za vyoo na sifa za choo bora. (angalia sura ya nne)
 2. Mjadala juu ya matatizo yanayokwamisha Revolving Fund (angalia sura ya nne)
-
- 27/5/92
1. Kutayarisha mipango ya kazi kwa kila mkoa/wilaya
 2. Kuunda 'Cobasheca' Club
 3. Mjadala juu ya Wakunga wa Jadi
 4. Kutayarisha malengo ya binafsi kwa mwaka 1992/93
 5. Kutembelea kijiji cha Bwina
-
- 28/5/92
1. Kujenga mabanda ya vyoo (superstructure) katika kijiji cha Bwina. (Tazama taarifa ya Sanitary Engineer).
 2. Kujadili matokeo ya tathmini ya warsha na kufunga warsha.
-

ORODHA YA WASHIRIKI WA AFYA - CHATO

1.	F. B. Kalimanzira	RHO	Mara
2.	F. Musira	PHNO - RTOT	Mara
3.	M. M. Kishumba	H/O - RTOT	Mara - (Secretary)
4.	E. Marwa	MCHA - DTOT	Sengerema
5.	A. Masige	PHNO - DTOT	Bunda
6.	H. Sarongo	MCHA - DTOT	Musoma (R)
7.	A. Lukwatage	NO - RTOT	Kagera - (Secretary)
8.	P. Rwekaza	H/O - DTOT	Muleba
9.	S. Rutta	PHNO - DSHPC	Biharamulo
10.	D. Misinde	RHO	Mwanza
11.	V. Ndalaha	NO - RTOT	Mwanza
12.	M. Sadataley	H/O - RTOT	Mwanza
13.	S. Ntomola	H/O - RTOT	Mwanza
14.	S. M. Kunaga	H/O - DTOT	Mwanza (Secretary)
15.	A. Kiteleja	H/A - DTOT	Kwimba
16.	M. Mayala	H/O	Kwimba
17.	T. Lukonge	PHN - DTOT	Ukerewe
18.	N. Simon	M/A - DTOT	Geita
19.	J. Bahati	M/A - DTOT	Sengerema
20.	S. Kilunga	H/A - S/TOT	Magu

Wakufunzi

Dr. E. S. Mwashu

HEA - Mwanza

Maoni ya Jumla

1. Kuhusu Choo Bora

Kuna umuhimu wa kuchukua takwimu za vyoo kutokana na sifa zake zilizotajwa pamoja na ainisho la choo bora.

Nani afanye: WAV, SubTOT na DTOT

Lini: Kabla ya mwisho wa 91/92 mwaka wa fedha

2. Usafiri

Magari ya mradi wa HESAWA badala ya kuuzwa kwa watu binafsi yatolewe kwa serikali za Halmashauri za wilaya zinazohusika ili yasaidie uendeshaji hata baada ya phasing-out.

Sababu kubwa ni kwamba Halmashauri za wilaya mara nyingi zina magari mazee ya miaka zaidi ya kumi, iwapo gari la mradi litamaliza miaka mitatu na kuuzwa basi litakuwa ni jipya kwa halmashauri za wilaya. Pia watekelezaji wapewe umuhimu wa pili wa kuuziwa magari hayo kama motisha.

3. Mradi wa afya mashuleni una lengo la kuhamasisha jamii katika kutambua, kupanga, kutekeleza na kutathmini matatizo yake. Wanawarsha wamesoma na kujadili na kuamua kuwa kabrasha la afya shuleni (SHP) linayo mambo yote muhimu na linafaa kutumiwa katika mradi wa HESAWA.
4. Ili kuhakikisha kuwa jamii inahusishwa kikamilifu katika utekelezaji wa mradi, Chato Convention tunapendekeza kuwa mradi unapoingia katika kijiji, mwaka wa kwanza utumike kuhamasisha na kutoa elimu ya afya halafu miaka inayofuata ndio shughuli za usambazaji maji na nyinginezo zifanyike.
5. Makisio ya Delivery Kit (visanduku vya kuzalishia) kwa ajili ya wakunga wa jadi yawepo na pia vifaa vya uzalishaji vinavyopatikana umuhimu wa kwanza wapewe wakunga wa jadi.

SURA YA KWANZA

A STUDY ON THE ROLE OF VILLAGE HEALTH WORKERS AND THE REVOLVING FUND IN THE HESAWA SANITATION STRATEGY (BY. Dr. E. S. Mwashu)

Washiriki walipewa taarifa juu ya utafiti uliofanyika kuhusu utendaji kazi wa WAV pamoja na usafi wa mazingira. Taarifa hiyo ilionyesha matokeo ya utafiti juu ya WAV na viongozi wa serikali za vijiji vyao. Matokeo ya vikao vya walimu na wasimamizi wa shughuli za WAV ngazi za wilaya, mkoa na vituo vya afya na matokeo ya focus group discussions.

Washiriki waligawanyika katika makundi ya mkoa kujadili taarifa hiyo na kufikia ufumbuzi wa baadhi ya matatizo yanayokwamisha utekelezaji wa shughuli za WAV.

Ili vikundi vijadili kikamilifu taarifa hiyo, mchokozi wa warsha alitoa maswali yafuatayo:

1. Kuainisha kwa undani zaidi maana ya neno "Sanitation"
- 2.1 Kwa nini utekelezaji wa sera ya usafi wa mazingira uko nyuma?
 - Taja matatizo yanayokwamisha
 - Yaweke matatizo yaliyotajwa kufuatana na umuhimu wa kila tatizo - Problem ranking
- 2.2 Jadili sababu zonazofanya matatizo yaliyotajwa yatokeze - (underlying causes).
- 2.3 Jadili ufumbuzi wa kila tatizo lililotajwa.
 - Kipi kifanyike?
 - Nani afanye?
 - Lini na namna gani kifanyike?

Yafuatayo ni matokeo ya mjadala wa vikundi vyote kwa ujumla

1. USAFI WA MAZINGIRA

Usafi wa Mazingira ni kudhibiti unadhifu na ubora wa vitu vyote vinavyomzunguka mwanadamu ambavyo vinazweza kuathiri afya yake k.m. hewa, maji, chakula, nyumba, bustani, choo, bafu, vichanja, mashimo ya taka n.k.

2. MATATIZO YANAYOSABABISHA USAFI WA MAZINGIRA KURUDI NYUMA NI KAMA YAFUATAYO

1. Wananchi hawaoni kama uchafu wa mazingira ni tatizo kwao.
2. Usimamizi na ufuatiliaji mbaya.
3. Uongozi hafifu katika ngazi zote.
4. Kutowajibika kwa watekelezaji.
5. Upungufu wa vifaa vya ujenzi vya asili.
6. Wahudumu wa Afya Vijijini hawathaminiwi na uongozi.
7. Upungufu na ukosefu wa watumishi.

8. Kuwepo kwa udongo tifutifu, majimaji, miamba ni mikubwa.
9. Hali duni ya uchumi.
10. Mhisani (HESAWA) kuthamini zaidi miradi ya maji kuliko usafi wa mazingira.
11. Muda wa mafunzo rejea/awali ni mfupi (hautoshi kufuatia sera za Wizara ya Afya).
13. Ushirikiano hafifu kati ya idara na idara pamoja na wahisani wengine.

MATATIZO NA SABABU ZAKE

TATIZO LA 1: Wananchi hawaoni kama uchafu wa mazingira ni tatizo kwao.

Sababu: a) kutoelewa (ujinga)
 b) mila na desturi
 c) poor approach
 d) elimu duni ya Afya
 e) kutokuwa na mbinu sahihi za ufundishaji (poor teaching methods)

Ufumbuzi: Elimu ya afya itiliwe mkazo zaidi katika mambo yafuatayo:

- a) kuelimisha watumishi juu ya Adult Learning na PBL katika ngazi zote mara mbili kwa mwaka kwa muda wa siku 5 (semina)
- b) kuendesha semina kwa viongozi wa vijiji mara mbili kwa mwaka (kila semina siku 2).
- c) kufanya mikutano ya hadhara kwa wananchi vijijini kwa muda wa siku moja, hii ifanyike mara mbili kwa mwaka
- d) somo la elimu ya afya liingizwe/litiliwe mkazo katika mitaala ya shule za msingi.
- e) wahudumu watembelee vijiji vyao mara tatu kwa wiki.
- f) TBAs na THs watumike kutoa elimu ya afya.

Nani afanye:

- a) RTOTs, DTOTs, and Sub TOTs
- b) SubDTOTs
- c) RTOTs, DTOTs, SubTOTs na Waalimu
- d) WAV
- e) TBAs na THs

Lini: Kuanzia 1st July 1992

TATIZO NA.2 : Usimamizi na ufuatiliaji mbaya

Sababu a) Ukosefu wa usafiri kwa ngazi zote
 b) Ukosefu wa posho, mafuta na vipuri
 c) Ugawaji mbaya wa nyenzo za usafiri unaofanywa na ofisi ya Kanda
 d) Ununuzi wa baiskeli ni mbaya (baiskeli za Gazeera hazifai).

- e) Uzembe wa baadhi ya watekelezaji
- f) Baadhi ya viongozi wa vijiji na wa ngazi nyingine za juu hawathamini shughuli za usafi wa mazingira.
- g) Kutokuwa na kalenda ya kazi.

Ufumbuzi:

- a) Kila kituo cha mafunzo kipewe pikipiki moja (in-charge wa shughuli za HESAWA)
- b) Kila DTOT apewe pikipiki
- c) Kila RTOT apewe pikipiki
- d) Kila mkoa upate gari moja kwa ajili ya shughuli za afya
- e) SubDTOTs wauziwe baiskeli kwa 25% badala ya 75%
- f) WAV wauziwe baiskeli aina nyingine bora zaidi ya Monark na Gazzebo k.m. Phoenix, Roadmaster.
- g) Fedha iliyopo kwenye halmashauri zisitumike kwa matumizi nje ya yale yaliyokusudiwa
- h) Mikoa ihusishwe na kanda wakati wa ugawaji wa nyenzo za usafiri na vifaa vingine muhimu (kanda iweke mwongozo wa ugawaji).
- i) Kila mtekelezaji aandae ratiba ya kazi na ifuatwe (hii iandaliwe katika ngazi zote).

Nani afanye: a) mpaka f) (usafiri) - HDD/SIDA
 (g) RDD, DED, RHC, DHC
 (h) HDD
 (i) RTOTs, DTOTs, SubDTOTs, na VHWS
 Lini: Kuanzia July 1992.

TATIZO NA. 3: Uongozi hafifu katika ngazi zote

Litafutiwe ufumbuzi

TATIZO NA 4: Kutowajibika kwa watekelezaji

- Sababu
- a) Ukosefu wa usafiri
 - b) Ukosefu wa motisha (lunch allowance)
 - c) Kutothaminiwa kwa budget za Afya
 - d) Uchaguzi mbaya wa baadhi ya watekelezaji wa mradi
 - e) Ukosefu wa ufuatiliaji kuanzia ngazi za kanda - mkoa - wilaya - tarafa - kata - kijiji - kata.

Ufumbuzi:

- a) Angalia ufumbuzi wa tatizo na. 2
- b) Makisio ya posho ya chakula cha mchana yafanyike kwa ajili ya wanaokwenda vijijini
- c) Yaanzishwe mashindano ya usafi wa mazingira katika ngazi ya kijiji, kata na wilaya na mshindi apewe zawadi maalum kama inavyofanyika kwa wenzetu wa idara za Maji na Maendeleo ya Jamii
- d) Wakuu wa Idara washirikishwe katika kukamilisha makisio yaani wawepo kama kuna umuhimu wa kupunguza baadhi ya miradi ya idara zao.
- e) Mkoa wa Mwanza una tatizo la usafiri kwa vile kuna mawazo kuwa ni rahisi kupata magari toka ofisi ya kanda Ofisi ya mkoa iwe na magari yake kama mikoa mingine.

- f) Tuwe na malengo ya kazi na watekelezaji watakaoshindwa kufikia malengo hayo wachukuliwe hatua za kinidhamu.
- g) Uwepo ufuatiliaji wa karibu zaidi kuanzia kanda hadi kaya.

Nani afanye:

- a) HDD/SIDA
- b) Wakuu wa Idara
- c) HDD/RDD/ DED
- d) HDD/RDD
- e) HDD/RHC
- f) Wakuu wa Idara, RTOTs, DTOT, SubDTOT
- g) Kanda - VHW

Lini: Kuanzia 1st July 1992

TATIZO NA. 5: Upungufu wa vifaa vya ujenzi vya asili

- Sababu a) Uharibifu wa mazingira (kukata miti ovyo na kutopanda miti)
- b) Umaskini

Ufumbuzi:

- a) Kuwaelimisha wananchi wasikate miti ovyo na wapande miti
- b) Wananchi waanzishe vitalu vya miche na hatimaye miche hiyo isambazwe. HESAWA ianzishe revolving fund kwa ajili hii.
- c) Wananchi waelimishwe namna ya kuanzisha na kuendesha miradi midogo midogo ya kuinua uchumi wao.
- d) Sera ya taifa ya upandaji miti ifuatwe.

Nani afanye: Wataalam wa Maliasili, Maendeleo ya Jamii, viongozi wa chama na serikali, shule, kilimo na wananchi wenyewe na hii ifanyike kuanzia July 1992.

TATIZO NA. 6: Viongozi kutowathamini WAV

- a) Baadhi ya Viongozi hawajahamasishwa kuhusu umuhimu wa WAV
- b) Wananchi walio wengi wanathamini zaidi shughuli za afya tiba kuliko kinga.

Ufumbuzi:

a + b Suala hili litiliwe mkazo katika semina za wanavijiji, pia katika vikao vyao vya HAM

Nani afanye: SubDTOTs, DTOTs, DPT, DPO, VHWS na hii ifanyike kuanzia July 92.

TATIZO NA. 7: Upungufu na ukosefu wa watumishi

- Sababu a) Mgawanyo mbaya wa watumishi wanaoshughulikia usafi wa mazingira vijijini
 b) Kutokuwa na maombi ya watumishi wakati wa makisio ya kila mwaka

Ufumbuzi:

- a) Uwepo mgawanyo mzuri wa watumishi
 b) Watumishi waombwe wakati wa makisio ili kukidhi matakwa ya sehemu hiyo.

Nani afanye: RDD/DED, RMO, RHO, DMO na DHO
 Lini: Kuanzia July 1992

TATIZO NA. 8: Udongo tifutifu, majimaji na miamba mikubwa

Ufumbuzi: Mhandisi wa usafi wa mazingira (Programme Sanitary Engineer) ashughulikie suala hili

TATIZO NA. 9: Hali duni ya uchumi

- a) Hali mbaya ya hewa
 b) Ujinga
 c) Ukosefu wa ardhi
 d) Kilimo cha kizamani
 e) Sherehe zisizo na mpangilio
 f) Michango mingi
 g) Familia kubwa
 h) Uzembe
 i) Maradhi
 j) Mazingara - imani za uchawi
 k) Uongozi mbaya wa baadhi ya serikali za kijiji

Ufumbuzi:

- a) Tupande miti
 b) Elimu ya kilimo bora itolewe, matumizi mazuri ya mapato yao na uzazi wa mpango.
 c) Kuwaelimisha wananchi waondokane na uzembe, ulevi, mazingara, maradhi na umaskini
 d) Viwepo vifaa vya kufundishia e.g. film projectors, video set, camera, flip charts, newsprint n.k.
 e) Wananchi wahamasishwe na washirikishwe kikamilifu katika kupanga kutekeleza na kutathmini shughuli zao za maendeleo

Nani afanye:

- a) Wataalam wa misitu, shule, idara nyingine na wananchi
 b) TBAs, THs, WAV, MCHA na watumishi wengine wa zahanati.
 c) HDD/SIDA
 d) Kamati za maendeleo za kata, Sub-DTOTs, DPT.

Hii ianze kufanyika July 1992.

TATIZO NA. 10: Mhisani (HESAWA) kuthamini zaidi maji kuliko usafi wa mazingira

- Sababu a) Kihistoria mradi ulikuwa wa maji na fikra hizo bado hazijabadilika kwa baadhi ya viongozi wa ngazi za juu
 b) Nembo ya HESAWA inaonyesha kuwa inajihusisha na maji peke yake.
 c) Shughuli za maji zinapewa asilimia kubwa zaidi na mradi kuliko shughuli za usafi wa mazingira.

Ufumbuzi:

- a) Ofisi ya kanda ibuni mbinu za kuondoa tofauti hii
 b) Nembo ibadilishwe ili kuonyesha shughuli zote za mradi
 c) Uwepo uwiano mzuri wa mgawanyo wa fedha na vifaa vingine

Nani afanye:

- a) HDD
 b) SIDA/HDD
 c) RDD/RHC, DED/DHC

Lini ifanyike: 92/93 financial year

TATIZO NA. 11: Muda wa mafunzo ya awali/rejea hautoshi

- Sababu a) Kupunguzwa na kukatwa kabisa kwa budget bila sababu za msingi
 b) Uongozi wa kanda kuingilia mipango ya miradi ya wilaya na mikoa bila mawasiliano ya kutosha

Ufumbuzi:

- a) Watekelezaji washirikishwe kikamilifu kujadili budget hadi hatua ya mwisho
 b) Ofisi ya kanda iondoe vikwazo visivyo vya msingi katika kupitisha budget wakati wa kutekeleza kazi iliyopitishwa.

Nani afanye:

- a) HDD/RHC/DHC
 b) HDD/ZTO

Hii ianze kufanyika 1st July 1992

TATIZO NA. 12: Ushirikiano hafifu kati ya idara na idara, wahisani kwa wahisani

Sababu a) Idara na idara

Ubinafsi wa watumishi na kutothamini kazi za watumishi wa idara nyingine

Wahisani kwa wahisani

- a) Kila mhisani anayo kalenda yake ya kazi na madhumuni tofauti na mhisani mwingine
- b) Hakuna uratibu mzuri wakati wa kuwapokea, kuwapangia kazi na kuratibu utekelezaji wa kazi zao ili kuzioanisha kazi na kuleta ufanisi mzuri zaidi

Ufumbuzi:

- a) Mfumo wa 'HAM ufuatwe
- b) Madhumuni ya wahisani yaratibiwe na kuoanishwa ili yaweze kuleta ufanisi mzuri zaidi
- c) Uwepo utaratibu wa kuwapokea, kuwapangia kazi na kuratibu utekelezaji wa kazi za wahisani ili kuzioanisha.

Nani afanye:

- a) RC/RMO, DC/DMO
- b) RDDs
- c) Kamati ya HAM ya mkoa/wilaya

Hii ifanyike kuanzia July 1992

SURA YA 2

MPANGO WA ELIMU YA AFYA SHULENI.

Wanawarsha walijadili dhana ya kutumia Elimu ya Afya mashuleni kama chanzo cha kutambua matatizo ya jamii na njia ya kuyatatua. Na pia umuhimu wa kutumia njia sahihi za kuingia katika jamii ulijadiliwa ya kwamba wakufunzi lazima watumie LEPSA na PBL kutatua matatizo ya kijamii (angalia appendix 1).

MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

1. Kuendesha mkutano wa siku moja kwa kila mkoa kwa wafuatao:
 - a) RMO, REO, RHC, RDD, RSHPC
 - b) DMO, DEO, DHC, DED, DSHPC (Jumla 35)

Nani Afanye: RTOTs, Health Advisor
Lini: June 1992
2. Uchaguzi wa shule zinazohusika kila wilaya.

Nani afanye: DTOTs, DSHPC, DDSC
Lini: July, 1992
3. Kuendesha semina ya walimu, dispensary staff, health assistants, WAV na Afisa Elimu Sayansi Kimu (W) DDSC.

Nani afanye: RTOTs, DTOTs, SUB-DTOTs
Lini: July 1992
4. Walimu wa shule kwa kushirikiana na uongozi wa serikali za vijiji vyao wapange na kuitisha mikutano ya wazazi.

Nani afanye: Walimu, Sub-DTOTs, WAV, Uongozi wa serikali za vijiji
Lini: August 1992
5. Utafiti wa takwimu za awali

Nani afanye: Sub-DTOTs, WAV, Walimu wakuu kwa kutumia wanafunzi
Lini: August 1992
6. Kuanzisha club za Afya Mashuleni.

Nani afanye: Walimu, Sub-DTOTs, DTOTs.
Lini: August 1992 (Angalia Appendix 2)
7. Kuendesha vipindi vya afya madarasani na kuwapa wanafunzi (pre- na post - tests).

Nani afanye: Walimu, Sub-DTOTS, WAV

Lini: Kuanzia 1st September 1992 na kuendelea. Angalia kiambatanisho 3

8. Ufuatiliaji wa shughuli zote za Mpango wa Afya mashuleni.

Nani afanye: RTOTS, DTOTS, Sub-DTOTS, WAV, Afisa Elimu Sayansi Kimu (W) na Uongozi wa serikali ya kijiji.

Lini: Kuanzia July 1992

9. Utoaji na Upokeaji taarifa za kila mwezi.

Nani afanye: RTOTS, DTOTS, Sub-DTOTS, WAV, Afisa Elimu Sayansi Kimu (W) na Uongozi wa serikali ya kijiji.

Lini: Kila mwezi kuanzia October 1992

10. Tathmini

Nani Afanye: RTOTS, DTOTS, Sub-TOTS, WAV, Mwalimu Mkuu na Afisa Elimu S/Kimu (W).

Lini: Kila robo ya mwaka (i.e. mara 4 kwa mwaka).

MAMBO MUHIMU YA KUTATHMINI

- a) Pre- and post- results
- b) Kuangalia kama shughuli zote zilizopangwa zimetekelezwa kikamilifu.
- c) Kuangalia kama kuna mafanikio katika kuinua hali za afya ya wanafunzi na wanakijiji kutoka kwenye taarifa za WAV.

11. Kuweka malengo upya kwa kufuata matokeo ya tathmini.

Nani afanye: RTOTS, DTOTS, Sub-dTOTS, Walimu, School Health club, Afisa Elimu S/Kimu (W).

Lini: Baada ya matokeo ya tathmini.

SURA YA TATU

MWONGOZO WA SIDA KUHUSU USAFI WA MAZINGIRA

Wanawarsha walipata nafasi ya kujadili mwongozo wa SIDA kuhusu usafi wa mazingira. Mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na matatizo ambayo yametajwa katika mwongozo huo. Mwongozo huo umetaja matatizo manane kama ifuatavyo:

- Nanukuu: "1. there has been an over-emphasis on water supply at the expense of sanitation and health education;
2. sanitation and health education have been seen as separate components in water supply programmes rather than as integrated activities;
3. health care systems in many low income countries remain imbalanced in favour of curative services and urban areas while environmental health programmes - including efforts to promote hygiene are relatively neglected;
4. project and programmes are insufficiently based on local problem analysis, consultation and resource inventories, including human resources;
5. local communities are not sufficiently involved in programme planning, implementation and evaluation;
6. even where community participation has been emphasized women tend to have been neglected;
7. technologies affordable to poor households are neglected or completely excluded from most assistance programmes;
8. project documents are often too general and vague and need to be more specific especially with regard to health education, excreta disposal, wastewater drainage and involvement of different groups in the communities."

Tatizo 1: Mkazo mkubwa umewekwa zaidi katika shughuli za maji kuliko shughuli za afya na usafi wa mazingira.

Sababu a) Kihistoria, mradi ulikuwa unashughulika na maji peke yake na fikra hizi bado hazijabadilika kwa baadhi ya viongozi muhimu.

b) Matakwa (felt needs) ya wananchi wengi zaidi ni katika masuala ya maji ukilinganisha na suala la elimu ya afya na usafi wa mazingira.

- c) Kihistoria miradi mingi ya maji maamuzi yake huanzia ngazi za juu ambapo HESAWA pia imeanzishwa bila kutoa tofauti hiyo.
- d) Nembo ya HESAWA pia inachangia kupotosha fikra za watu kwa sababu inaonyesha shughuli za maji peke yake.

Ufumbuzi:

- a) Ofisi ya Kanda ibuni mbinu za kuondoa tofauti hii.

Nani Afanye: HDD (mwaka wa fedha 92/93)

- b) Mwaka wa kwanza mradi unapoingia kijijini utumike kuhamasisha wananchi na kutoa elimu ya afya, mwaka wa pili na kuendelea ndipo shughuli za usambazaji maji na nyinginezo zianze. Vijiji vitakavyoonyesha maendeleo mazuri katika shughuli za usafi wa mazingira vipewe kipaumbele katika masuala ya maji.

- c) Shughuli za uhamasishaji ziwe ni mini projects katika mradi mzima wa HESAWA na yawepoi malengo maalum, njia za utekelezaji zieleweke na pia tathmini ifanyike vizuri kupima mafanikio ya shughuli za uhamasishaji.

Nani afanye: HDD. SIDA, DPO na DPT
Lini : Kuanzia July 1992

Ufumbuzi wa sababu (b) na (c)

- a) Yawepo makisio kwa ajili ya kuendesha semina za wanavijiji ili kuwawezesha kupanga, kutekeleza na kutathmini shughuli zote za mradi.
- b) DPT members na DPO wapewe au wafundishwe mbinu za ufundishaji (adult teaching methods).
- c) Mshauri wa Afya wa mradi awashauri waganga wakuu wa mikoa na wilaya zinazohusika ili RTOTs na DTOTs wapewe muda wa kutosha wa kufanya shughuli za mradi.

Nani afanye kuhusu ufumbuzi a, b na c hapo nyuma?

- a) Idara zote zinazohusika na mradi kuanzia July 92
- b) HDD/HEA kuanzia July 92
- c) HEA July 92

Sababu 4. (Nembo ya HESAWA)

Ufumbuzi: Nembo ibadilishwe ili ionyeshe shughuli zote za mradi.

Nani afanye: HDD/SIDA
Lini: 92/93 (mwaka wa fedha)

TATIZO NA. 2:

Shughuli za Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira hazina uwiano na shughuli za maji katika mradi.

Sababu a) Shughuli za maji zinapewa kipaumbele na kuwa chanzo cha shughuli nyingine. Kwa sababu hiyo idara nyingine zinalazimika kuanza kazi katika maeneo hayo hata kama sio "felt needs" za wananchi.

Ufumbuzi: Mwaka wa kwanza shughuli za uhamasishaji kuhusu usafi wa mazingira zitiliwe mkazo zaidi ili kuweka mazingira yao katika hali ya usafi na kuwaelimisha kuwa maji yanaweza kuwa chanzo cha kueneza maradhi, na vijiji vitakavyoonyesha maendeleo mazuri katika usafi wa mazingira vitapewa kipaumbele katika kupewa visima.

Nani Afanye: HDD/SIDA (kuanzia July 92).

Ufumbuzi wa sababu b: Mradi uweke mkakati wa kuimarisha ushirikiano kati ya idara zinazohusika kwa kufanya mambo yafuatayo:

I. PROMOTION TEAM

a) Mpango wa kazi za promotion team upangwe kwa pamoja na nakala za mpango huo zitawanywe kwa idara zote zinazohusika.

Nani afanye: DHC/DPO July 1992

b) Teaching methodology ya DPT members iwe ni moja na katika uhamasishaji wao wawe na mwelekeo wa aina moja.

Nani afanye: DPT July 1992

II. DAT

a) DAT ikutane inavyotakiwa (mara moja kwa mwezi) na mpango wa kazi wa idara mbalimbali uanzishwe katika mikutano hiyo, nakala za mpango wa kila idara zisambazwe kwa DAT members wote.

Nani afanye: RDD/HDD July 92

TATIZO NA. 3 (katika mpango wa HESAWA hili sio tatizo)

TATIZO NA. 4

Utafiti wa Takwimu za awali (Detail Feasibility Study) haufanyiki kabisa kabla ya kuanza mradi katika eneo fulani.

Sababu a) Viongozi walioanzisha mradi walisahau umuhimu wa kufanya situational analysis.

b) Mwongozo na makisio ya mradi hauna kipengele kinachoruhusu wilaya kufanya situational analysis kabla ya kuingia katika maeneo mapya.

Ufumbuzi: Mwongozo wa makisio uwe na fungu maalumu kwa ajili ya situational analysis.

Nani afanye: SIDA/HDD kuanzia July 92.

TATIZO NA. 5

Jamii haihusishwi kikamilifu katika kutambua, kupanga, kutekeleza na kutathmini miradi yake.

Sababu a) Viongozi wa ngazi zote hawaamini kuwa jamii inaweza kupanga na kutekeleza miradi yake.

Ufumbuzi: Ifanyike semina maalum juu ya community participation kwa baadhi ya viongozi. Wafundishwe pia juu ya PBL na LePSA techniques.

Nani afanye: SIDA/HDD kuanzia July 1992

b) Watekelezaji hawajui mbinu za kushirikisha jamii katika upangaji na utekelezaji kimatendo.

Ufumbuzi:

i) Watekelezaji wafundishwe jinsi ya kufundisha na kuwasiliana na kina mama (adult teaching methods).

ii) Mbinu zilizotumika katika School health and sanitation package zinafaa sana kuhamasisha wananchi. Mbinu hizi zizingatiwe katika sehemu zote za mradi.

iii) Iwepo mikutano ya wanawake peke yao kuzungumzia masuala ya usafi wa mazingira.

Nani afanye: DPT, RTOT, DTOTs, VHW, SubTOTs, DPO
Lini: Kuanzia July 1992

TATIZO NA. 6

Ushirikishwaji wa wanawake katika kuamua, kupanga, kutekeleza na kutathmini miradi yao k.m. usafi wa mazingira.

Sababu a) Wataalam hawajui mbinu za kuingia katika jamii (community approach).

b) Kutokana na mila na desturi za kiafrika wanawake hawaongei mbele ya wanaume.

Ufumbuzi:

- a) Wataalam wafundishwe jinsi ya kufundisha na kuwasiliana na akina mama (adult teaching methods).
- b) Iwepo mikutano ya wanawake peke yao kuzungumzia masuala ya usafi wa mazingira.

Nani afanye: DPT, ROT, STOTs, VHW, SubTOTs na DPO.
Lini: Kuanzia July 1992.

TATIZO NA. 7

Appropriate Technology katika usafi wa mazingira haizingatiwi ipasavyo e.g. ujenzi wa vyoo vya mabamba.

Sababu a) Utaalamu na ufundi (technology) hubuniwa katika ngazi za juu na kuletwa kwa wananchi bila kujali gharama zake, mila na desturi zao.

Ufumbuzi: Ufanyike utafiti juu ya mila na desturi za watu na raslimali zilizopo katika jamii kabla ya kuamua tecknolojia itakayotumika katika jamii inayohusika.

Nani afanye: SIDA, PE, HDD, SE na watekelezaji wengine.
Lini: July 92

TATIZO NA. 8

Tatizo hili halikujadiliwa.

SURA YA NNE

VYOO BORA NA REVOLVING FUND

Wanasemina walijadili taarifa ya P. Morgan kuhusu takwimu za vyoo, ikaonekana kuwa idadi ya vyoo iliyoandaliwa ili kufikia uamuzi kuwa sanitation iko nyuma sio sahihi kwa vile inalenga mambo machache tu yafuatayo:

- a) Vyoo vilivyotolewa taarifa ni vile vyenye slab tu na ambavyo vimejengwa chini ya mradi wa HESAWA vikiwa na vent pipe
- b) Idadi iliyoandaliwa ni kutoka eneo moja tu na wala sio kuwakilisha wilaya/mkoa mzima. Kwa mfano, idadi ya vyoo vya wilaya ya Bunda ni ile ya kijiji cha Kitaramanka peke yake.

Baada ya hayo sifa za choo bora ziwe ni vigezo vya kuamua idadi ya vyoo bora/vibovu katika maeneo yote yanayoshughulikiwa na mradi.

Uamuzi wa kuwa na sanitation bora au mbaya ufikiwe baada ya kuangalia idadi ya vyoo bora vyote vilivyoko katika maeneo ya mradi na wanasemina walikataa kabisa fikra za kusema kuwa choo bora ni chenye slab ya cement na vent pipe.

Hivyo wanasemina walisema kuwa sifa za choo bora na ainisho la choo bora ni kama ifuatavyo:

1. Kina - Futi 12 +
2. Sakafu - Imara (yenye magogo, vyuma, sementi) inayoweza kuwekwa katika hali ya usafi isiyo na nyufa iliyo inuliwa
3. Kibanda - chenye kuta imara (zenye udongo, miti ya kusilibwa, mabati, matofali) chenye mlango (privacy) kiwe kirefu - mtu mzima aingie bila shida kiwe na eneo la kutosha
4. Paa - Paa imara (yenye nyasi, bati, vigae) Isiyovuja Iwe na slope ya kurusha maji nje
5. Inaweza kuwekwa venti au isiwe na venti

Ainisho

Choo bora ni kile ambacho ni imara ambacho hakina harufu au hakiruhusu kuzaliana kwa mainzi na kinaweza kuwa na venti au kisiwe na venti.

Revolving Fund

Tatizo: Revolving fund haizunguki

- Sababu**
- a) Top down introduction of RF
 - b) No anthropological studies done to identify acceptable and affordable types of latrines
 - c) Neither promotion nor community involvement done before introducing RF
 - d) Vifaa vya kuiwezesha izunguke havipatikani kutoka CD Store
 - e) Uchunguzi juu ya gharama za ujenzi wa vyoo haukufanyika i.e. understructure slab
 - f) Sera ya usafi wa mazingira ya mradi haelezi kikamilifu jinsi ya kuendesha RF

Ufumbuzi:

- a) Wananchi washirikishwe katika kuchagua teknolojia ya kutumika na kutambua rasilimali zilizopo kabla ya kufanya makisio ya RF
Nani afanye: DPT, DTOTs, Sub-DTOTs, VHWS
- b) Ofisi ya kanda iweke makisio ya kufanya Anthropological studies
Nani afanye: HDD, Planning and Evaluation Unit
- c) Angalia taarifa juu ya Sanitation Package. Utaratibu huu mzuri wa kuingia katika jamii ufuatwe.
- d) Ofisi ya kanda iweke mfumo mzuri ili vifaa vipatikane kutoka kwenye mradi na CD Store

Nani afanye: HDD/ STM (Stores and Transport Manager)
AU

Vijiji vipewe vifaa vya kutosheleza asilimia 50% ya mahitaji

Nani afanye: SIDA/Serikali
AU

Mabamba na vifaa vingine vya ujenzi vitolewe bure kwa sehemu zisizo na miti na kuliko na miti, mradi usaidie kutoa usafiri wa kuisomba

Nani afanye: HDD/SIDA

- e) Uchunguzi juu ya gharama halisi za ujenzi wa vyoo vya aina mbali mbali ufanyike kulingana na wakati uliopo.

Nani afanye: Sanitary Engineer, RTOTs na DTOTs

- f) Sera ya Usafi wa mazingira izingatie vyema ufafanuzi juu ya kuendesha RF.

Nani afanye: SIDA, HDD na HEA
Hizi zifanyike kuanzia July 1992

SURA YA TANO

MENGINEYO

Washiriki waliweza kujadili mambo kadhaa ikiwa ni mengineyo. Yaliyojadiliwa yalikuwa kama ifuatavyo:

1. Jinsi shughuli za Usafi wa Mazingira na elimu ya afya zitakavyoendesha baada ya eneo kuwa phased-out
2. Kuunda COBASHECA Club
3. Nafasi ya wakunga wa jadi katika jamii na mradi
4. Mipango ya utekelezaji ya mikoa
5. Tathmini

1. SHUGHULI ZA USAFI WA MAZINGIRA NA ELIMU YA AFYA ZITAKAVYOENDELEA BAADA YA ENEO KUONDOKA KWENYE MRADI WA HESAWA

a) Usafiri

- i) DEDs wahimizwe ili waweze kusaidia katika usafiri
Nani Afanye: RDD, RMO, RTOT
- ii) Kujenga tabia ya ushirikiano na idara nyingine ili usafiri mdogo uliopo utumike kwa wote.
Nani afanye: RDD, RMO, DED, DMO
- iii) Vyombo vya usafiri vya mradi vilivopo wilayani na mikoani vibaki huko badala ya kuuzwa. Ikibidi idara hizo zipewe kipaumbele
Nani afanye: SIDA/HDD
- iv) Watekelezaji wa mradi wawe na moyo wa kutumia vyombo vya usafiri walivyonavyo hata baada ya mkataba kumalizika.
Nani afanye: DTOTs, RTOTs, and SubDTOTs
- v) Sub-DTOTs na Dispensary staff waendeleo kuwa wasimamizi wa shughuli zote za Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira.
- vi) Magari ya HESAWA yakabidhiwe wilayani badala ya kuyauza yanapomaliza miaka mitatu katika mradi.

b) Mapendekezo mengine

